# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA
# SHULE YA SEKONDARI KABUNGU


Namba za simu

Shule ya Sekondari Kabungu,
S.L.P 532,
Mpanda-Katavi.

Mkuu wa shule: 0684341309/0756538662

Makamu Mkuu wa Shule: 0759284251/0623259351

Muhasibu wa shule: 0756950396/0623382941

Email: kabusec@gmail.com


10/03/2024

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi: ……………………………

S.L.P …………………..

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KABUNGU. HALMASHAURI YA WILAYA YA TANGANYIKA- MKOA WA KATAVI- MWAKA WA MASOMO 2024/2025**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka huu wa masomo 2024/2025 kwa tahasusi ya………………………………. katika Shule ya Sekondari Kabungu. Shule hii ipo umbali wa Kilometa 10 Magharibi mwa Mji wa Mpanda. Ina tahasusi za HGL, HGK, CBG, PCB na PCM.

## A. USAFIRI KUTOKA MIKOA MBALIMBALI

Kila mwanafunzi atajitegemea usafiri. **Usafiri wa GARI MOSHI toka Tabora kuja Mpanda** upo kila **Jumatatu**, **Jumatano** na **Jumamosi**, na gari moshi hufika Mpanda siku za **Jumanne**, **Alhamisi** na **Jumapili**.

Pia usafiri **wa mabasi** upo kila siku. Usafiri wa **mabasi** kutoka **Mbeya hadi Mpanda**, unapatikana kila siku kwa mabasi ya **Ruchoro Express, bubele express, sadi express na ngotico express**. Kutoka **Arusha - Mpanda** kuna mabasi ya kampuni moja tu ya uhakika ambayo ni **Mumuk**. Kutoka **Mwanza hadi Mpanda** kila siku kuna, **ALLYS STAR, Esanda express, Nyehunge express na Premier line**. Na kutoka Kigoma kuna mabasi ya kampuni za **Adventure Connection, combas express na Superdoll**.

**Dar es salam kuja Mpanda kuna mabasi ya <u>happy nation, A. N.  class, na bubele logistic</u>**

Kutoka sumbawanga kuna  mabasi ya **<u>princes j., ruchoro expres, na chakito express</u>**

Pia kuna usafiri wa **Ndege za kampuni ya ATCL** ambazo hufanya safari zake siku za **Jumanne, Alhamis** na **Jumamosi** kutoka **Dar es Salaam** kuja mpanda

**B. USAFIRI BAADA YA KUSHUKA STENDI KUU MJINI MPANDA**


usafiri wa mabasi,bajaji na pikipiki unapatikana katika kituo cha mabasi Mpanda Mjini nauli ni **Tsh. 2,000/=kwa daladala na tshs 4,000/= kwa bajaji na kwa pikipiki(bodaboda) haizidi 6000/= (angalizo; usikodi bodaboda usiku, usije na simu eneo la shule ni kosa)**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …**/…/2024.** Hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…/../2024**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **…/…/2024. kuripoti ndani ya wiki mbili (2) tangu muhula wa masomo kuanza ni vema zaidi maana baada ya muda huo kupita nafasi yake yaweza kuchukuliwa na mwanafunzi mwingine.**

**Ni vyema kuwasiliana kabla ya kuanza safari.**

***MOTO WA SHULE: ELIMU NI KINGA***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**



**ABDALLA DAWA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KABUNGO
MPANDA

1. **Mambo muhimu yakuzingatia**
   - **1.1 Sare ya Shule**
   - **1.2 DARASANI.**
     a) Suruali **ya dark blue mbili (2)** na **nyeusi mbili (2)**
     b) Mashati mawili **meupe** mikono mirefu
     c) Fulana (T-shirt) ya darasani moja (1) rangi ya **light blue** yenye nembo ya shule.

d) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na Soksi jozi mbili nyeusi.(aje navyo)

e) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.(aje nao)

f) Sweta moja (01) rangi ya **damu ya mzee**

g) Tai rangi ya **dark blue** mbili (02) na nyeusi mbili (2).

**1.3 KAZINI**

(a) Suruali za kushindia (Shamba dress) **mbili (2) rangi ugoro.**

(b) Fulana moja (01) rangi ya **njano** yenye nembo ya shule.

**1.4. MICHEZO**

(a) T-shirt moja na bukta yake nyeupe yenye nembo ya shule.

(b) raba nyeusi( aje nazo)

**1.5. MAANDALIO YA KUSOMA.**

Track suit jozi moja ya rangi **nyeusi yenye nembo ya shule** kwa ajili ya maandalio ya kusoma wakati wa usiku.

**1.6. MALAZI.**

(a) Shuka mbili (2) rangi ya **pinki**

(b) foronya mbili (2) za **pinki**. (aje nazo)

(c) Chandarua

(d) Godoro futi $2^1/_2$.

(d) blanketi la kujifunika la rangi yoyote (aje nalo)

**1.7. NJE YA SHULE**

(a) Mwanafunzi akiwa safarini au nje ya shule atavaa suruali nyeusi na fulana (**t-shirt) ya dark blue yenye nembo ya shule** na viatu vya darasani.

**(b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni ni:-.**

**i.** madaftari 10 ya counter books 3 or 4 quire

**ii. Ream 2 ( A4)** ya karatasi (kwa mwaka

**iii**. Vitabu vya masomo ya tahasusi anayosoma.

**iv**. kwa wale wasio na bima ya afya ya **NHIF** waje na fedha ya bima ya afya kwa mwaka ni. **NHIF TSHS: 50,400/=**
**(aje nayo mkononi)**

**V. scientific calculator (**kwa wanaosoma hesabu)

**NB;-**

Si jukumu la shule kushona sare za wanafunzi, bali mwanafunzi ataelekezwa kwa fundi alieteuliwa na shule, utaratibu huu ni mhimu ili kufanya wanafunzi wawe na sare zenye kufanana. Kama mzazi ameamua kumshonea au kumnunulia mtoto wake sare tajwa hapo juu na zika tofautiana na shule basi mzazi atalazimika kushona nyingine.

**03. michango ya shule.**

**a)** Michango ya shule ina jumla ya tshs:80,000/= . Fedha hizo zilipwe kupitia Akaunti ya shule **KABUNGU SECONDARY CAPITATION ACCOUNT Na. 61901200065** katika benki ya **NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in Slip)**

**(b) MCHANGANUO WA MICHANGO YA SHULE**.

| S/N. | AINA YA MICHANGO | MALIPO KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1 | UENDESHAJI WA SHULE | 65,000/= |
| 2 | TAHADHARI | 5,000/= |
| 3 | NEMBO | 5,000/= |
| 4 | KITAMBULISHO CHA SHULE | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

***NB:MICHANGO YOTE INAPASWA KUWEKWA KATIKA AKAUNTI ILIYOANDIKWA HAPO JUU.***

**ORODHA YA VITABU**

**GENERAL STUDIES**

1. Richard, R.F. Mbalase. **General Studies For Advanced Level Certificate**;
2. Mgaywa, B.M. **General Studies for Advanced level 3rd Ed**.
3. Joannes Bigirwa Mungu & Sospeter.M. Deogratias. **Understanding Advanced Level general Studies;** Advanced Secondary School Education;

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

1. Basic Applied Mathematics for Secondary School.
2. Basic Applied Mathematics Review.
3. Basic Applied Mathematics (TIE)

**PHYSICS**

1. Mehta, R. and V. K Mehta (2009) *"Principles of Physics for Class XI*" New Delhi, S.Chand and Company Ltd.
2. Nelcon, M and P. Parker (1995) *"Advanced level Physics''* 07th Edition, London, Heinmann Educational books.
3. TIE (2019) "*Physics for Advanced Level Secondary Schools*, Form Five, Dar es salaam, TIE.

**CHEMISTRY**

1. Jain s.k (2006) *Conceptual Chemistry XI ,4th edition*. Chand, New delhi India
2. Ngaiza lusima (2014) *Atomic Structure and Bonding*. Hopegen company ltd. Dar es salaam. Tanzania
3. Ngaiza lusima (2014*) Physical Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
4. Ngaiza lusima (2014) *Inorganic Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
5. Ngaiza lusima (2014) *Environmental and Soil Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania.
6. E. Ramsden (2001) *Calculations for A-level chemistry*.

**ADVANCED MATHEMATICS**

1. Pure mathematics 1&2 by Back House & SPT Houldsworth,
2. Pure mathematics by Bostock
3. Concise course in statistics by J. Chamber

**BIOLOGY**

1. Biology for Class xi and Class xii by Dr. P. S. Verma & Dr. B. P. Pandey S. Chand's
2. Biological science by D. J. Taylor,
3. New understanding Biology for Advanced level fourth edition by Glenn and Susan Tool
4. Dissecting kit na Tray kwa wanafunzi wa Biolojia( Tahasusi ya PCB na CBG)
5. Scienitific Calculator

**GEOGRAPHY.**

1. Pritchard J.M (1979). Afric A study of Geography for Advanced Students. London Longman
2. Msabila D.T (2003), Success in Geography Climatology and social science. Dar res salaam. Afroplus Industries.
3. Pritchard J.M.(1990), Practical Geography for Africa. Longman.
4. Kamil, Z. Physical Geography; Dar es salaam. Afroplus.
5. Msabila D.T. Physical Geography. Dar es Salaam. Nyambari Nyangwine Publishers.
6. Msabila D.T.(2006) Hhuman Geography (Advanced level paper 2). Nyambari Nyangwine Publishers.

**VITABU VYA HISTORY: -**

1. Bigirwamungu, J & Deogratias M. (2015) *Understanding African History*,Paper 1, New Version, Mikumi Publishers.

2. Kato, A.K. (2012) *Mastering Advanced Level History Book*, Mwanza, Mweas Book Publishers

3. Kato, A.K (2012) *Mastering Advanced Level History Book 2*, Mwanza, Mweas Book Publishers

4. Samwel, S & Stephen. O (2008) *World History Advanced Level*, Dar es salaam, Nyambari Nyangwine Publishers.

5. Shibitali, C.K (2017) *Contemporary Historical Events,* Third Edition, Dar es salaam, Che Guevara Investment.

6. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 1*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press.

7. Yassin,S.(2015) *Essentials in Advanced Level History Paper 2*, Dar es salaam, Ahmaddiya Printing Press .

8. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools Form Five*, Dar es Salaam, T.I.E.

9. Tanzania Institute of Education (2010) *History for Secondary Schools*, Form Five, Dar es Salaam, T.I.E

**VITABU VYA KISWAHILI**: -

1. Masebo, J.A & Nyangwine. N (2010) *Tahakiki Kidato cha 5& 6.* Nyambari Nyangwine Publisher, Dar es Salaam.
2. Mwansoko, H.J.M (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri*, TUKI – Dar es Salaam.
3. Kihore. Y.M na Wenzake (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.
4. Massamba, D.P.B na Wenzake (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Sekondari na Vyuo*; TUKI Dar es Salaam.
5. Saluhaya, M.C (2010) *Nadharia ya Lugha Kidato cha 5 & 6.* S.T.C Publishers- Dar es Salaam.
6. Masebo.J.A & Nyangwine, N (2009) *Nadharia ya Lugha kidato cha 5 & 6* . Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.
7. Masebo, J. A & Nyangwine, N. (2008) *Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5 & 6*, Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.

**VITABU VYA SOMO LA KIINGEREZA**

1. Ndambo,G.S & Kinunda, J.E. (2017). *Advanced Level English Language 1*, Form 5&6. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

2. Kadeghe, M. (2010), *The Real English Textbook for Advanced Level,* Form Five, Dar es salaam, Jamana Printers Limited.

3. Kadeghe, M. (2010) *The Real English Textbook for Advanced Level*, Form Six. Dar es salaam, Jamana Printers Limited.

4. Asheli, N. (217) *Advanced Level English Language Structure & Stylistics*, Dar es salaam, APE publishers Ltd.

5. Lyi Kwei Armal, *the beautiful one are not yet born.*

6. Chunua Achebe, *A man of the people*

7. Heinrich Ibsen, *An Enemy of the people*

8. Ngungi wa Thiongo, *I will merry*

**NB;- si lazima kuja na vitabu tajwa hapo juu hii ni kwa yule ambae anauwezo wa kuvinunua na vitakuwa chini ya mtoto mwenyewe na ni mali yake.**

(a) Stop watch kwa wanafunzi wa taasusi ya PCM
(b) Disserting kit, Tray pamoja na Stop watch kwa taasusi ya CBG na PCB.

**VYOMBO VYA CHAKULA.**

(a) Sahani na kijiko
(b) Kikombe na bakuli.

**VITENDEA KAZI.**

(a) Ndoo ndogo mbili (2) za plastiki za lita kumi ( moja kwa matumizi ya shule).

(b) Kwanja (fyekeo)1, jembe1lenye mpini, fagio la ndani (soft bloom) 1, fagio kubwa ya chelewa (1), mopa kamilifu 1, panga au shoka 1, squeezer 1, hard brush **1.**

**MWANAFUNZI AJE NA RESULTS SLIP YA MATOKEO YAKE YA KIDATO CHA NNE.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi**

**kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5. Tafadhali soma kwa Umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KABUNGU SEKONDARI**

**ABDALLA DAWA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KABUNGU
MPANDA

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**i. MKUU WA SHULE : 0756 538 662/0625 895 681. ( Abdalla k. Dawa)**
**ii. MAKAMU MKUU WA SHULE: 0623 259 351/0759 284 251 (Endrausi D. Magidanga)**

**<u>ELEWA,</u>**
**Si rahisi kutunga sheria kwa kila kosa linaloweza kufanywa na mwanafunzi**

## 6. VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

### (a) REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

FROM THE HEAD OF SCHOOL,
KABUNGU SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 532,
MPANDA .

To the medical officer, ………………………………………………………………………
(Name in full)
Please examine the above named student as to his physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following categories (a-d).

a. (i Eyesight (ii)Hearing (iii)Speech (iv)Limbs (v)general diseases (vi)leprosy (vii)epilepsy.

b. Neurosis

c. Other serious diseases e.g. Asthma, T. B., etc.

Name………………………………………date………………………………signature……
……………….

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(i) Eyesight……………………………………………………………

(ii) Hearing…………………………………………………………

(iii) Speech……………………………………………………………

(iv) General diseases………………………………………………

(v) Leprosy………………………………………………………………

(vi) Epilepsy…………………………………………………………

(vii) Neurosis…………………………………………………………

(viii) Other serious diseases e.g. Asthma…………………………

(ix) T. B………………………………………………………………

Comments………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
Name……………………Date…………Signature……………**STATION**………………

**DESIGNATION………………………………..**

(b) **FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI, KUKUBALI SHERIA ZA SHULE NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**.

**(i)** ***<u>TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI</u>:***

1. JINA LA MWANAFUNZI:
   ………………………………………………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA:
   ………………………………………………………………………………
3. MAHALI ALIPOZALIWA:
   WILAYA…………………………………MKOA…………………………

4. MAHALI ANAPOISHI KWA SASA: MTAA………………………… KATA…………………………………… TARAFA: …………………………WILAYA: ……………………………………MKOA………………………………
5. URAIA: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA: ………………………………KABILA ……………………
6. SHULE NILIYOTOKA: ………………………………………………………………………………………
7. NAMBA YA MTIHANI (CSEE); …………….SHULE NILIYOFANYIA MTIHANI KIDATO CHA NNE…WILAYA YA: …………………………MKOA: ………………….

**(ii) KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA**.

MIMI …………………………KIDATO CHA…………MWAKA……………..MCHEPUO WA……………
Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.

TAREHE: ………………….SAINI: …………………………………

(c) **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:**
**MWANAFUNZI**:

Mimi:…………………………………………………………………………
Nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria, kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

**(d)** ***<u>TAARIFA YA MZAZI/MLEZI ;(ANDIKA MAJINA MATATU)</u>***

1. JINA LA BABA: ………………………………MAHALI ANAPOISHI: ………………….
YUKO HAI /AMEFARIKI …………………………KAZI YA BABA……………………………………… SIMU YA BABA……………………………S.L.P…………….MJI…………………………………………
2. JINA LA MAMA…………………………MAHALI ANAPOISHI …………………….
YUKO HAI /AMEFARIKI ……………………………KAZI YA MAMA:……………………………SIMU YA MAMA…………………………………………

S.L.P. ..........................MJI.........................................

**ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI**:

3. JINA LA MLEZI WA KIUME…………………………… MAHALI ANAPOISHI……………………
UHUSIANO……………………………………SIMU: …………………………………
JINA LA MLEZI WA KIKE ………………………………….MAHALI ANAPOISHI……………………UHUSIANO…………………………SIMU………………………
S.L.P. …………….MJI…………………………

**(e) <u>MZAZI/MLEZI (AZAJE SEHEMU HII):</u>**

Mimi……………………………………………………………………nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi…………………………………………na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri. Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo.

TAREHE……………………………………………………SAINI: …………………………

**(f) <u>SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU</u>:**

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.
MAJINA MATATU MFANO: ROSE ZABRON MUSSA.

| JINA | UHUSIANO: | NAMBA ZA SIMU: |
|---|---|---|
| 1. ……………………………. | ……………………….. | ……………………. |
| 2. ……………………………. | ……………………………… | ………………………… |
| 3. ……………………………… | ……………………………… | ………………………… |
| 4. ……………………….. | ……………………….. | ………………………… |

| PICHA YA BABA | PICHA YA MAMA | PICHA YA MLEZI | PICHA YA MLEZI |
|---|---|---|---|